Baada ya kimya kifupi Mzee Makete akasema, "Mpenzi, Kassim Hashir angali hai. Ndiye aliyenigonga."
"Nafahamu. Polisi tayari wanamtafuta."
"Huoni kuwa ni wajibu wetu kumweleza Denny ukweli?"
"Nimekwisha mueleza."
"Asante sana. Umenipunguzia mzigo mkubwa sana."
"Nimemweleza kila kitu, tangu mwanzo hadi mwisho. Hata jinsi alivyopata yale makovu."
"Akasemaje?"
"Unamjua jinsi Denny alivyo. Hakubadilika. Kama vile nimemsimulia kisa cha mtu mwingine kabisa."
"Kuna wakati mtoto huyo hunishangaza na kunitia wasiwasi."
"Si peke yako."
"Kama vile ana kasoro." Aliendelea Mzee Makete. "Kama vile si mtu wa kawaida!"
"Yaani taahira ?"
"Hapana. Hapana, Denny ni mzima kabisa. Ana akili kama mtu wa wastani. Isipokuwa ana tofauti kidogo na mtu wa kawaida. Hupenda kuishi porini, kufanya mazoezi magumu, kwake hakuna kinachomstua na haogopi kitu hata kama kwa wengine kitaonekana ni kigumu na cha hatari kiasi gani. Inatokana na viini vya chimbuko bila shaka. Yaani jenetiki."
"Tulifanya makosa kumchukua hali tukijua anaweza kuwa na jenetiki za Kassim Hashir?"
"No. Hapana. Hatukufanya kosa hata kidogo. Tusingemchukua sisi angechukuliwa na mtu mwingine. Au pengine angepelekwa kwenye makazi ya watoto yatima. Pengine asingepata malezi kama tuliyompa. Hapana, hatukufanya kosa hata kidogo kumchukua."
Bi mkubwa akashusha pumzi. Akasema, "Sijui ningejisikiaje ungesema tulifanya kosa. Unajua tumejizuia kuzaa kwa kuogopa kuja kugawa upendo. Hakuna wa kuthubutu kuninyang'anya Denny wangu. Hakuna." ,
"Mpenzi, mpenzi, mpenzi, hakuna wa kukunyang' anya Denny wako. Awe taahira, zuzu, awe na bongo au la ni wako. Kihaki, kisheria na Kimungu."

Kachero Koplo Koba alimuona daktari tangu alipozimaliza ngazi na kuingia kwenye korido. Alikuwa mgeni kabisa kwake, lakini tena, hakuwa akiwafahamu madaktari wote wa hospitali hii.. kubwa Isitoshe, hakuwa na tofauti yoyote na madaktari wengine. Kama ilikuwepo, basi ni ya huyu kuonekana ni daktari aliyekamilika. Alivaa kidaktari, pamoja na pimamoyo shingoni.' Na hata tembea yake ilikuwa ni ya kidaktari.

"Habari za hapa kijana?" Chox alitamka kwa sauti nzito, ya uhakika.

"Salama tu Dokta."

"Good, Very good." Chox alisema akiridhika kwa kichwa. "Dk. Makete yuko peke yake au kuna mtu mwingine ndani?"

"Yuko na mkewe. Amewasili sasa hivi."

"Good. Good. Very good."

Chox akapenya kwenye mlango uliokuwa wazi.

Akasema, "Shikamoo Mama Makete."

"Marahaba Dokta. Karibu"

"Asante." Alijibu Chox Akavichukua vyeti vya matibabu kitandani. Akauliza, "Anajisikiaje mgonjwa wetu?"

"Hajambo. Yuko macho."

"Good. Very good." Chox akavirudisha vyeti na kumkaribia mgonjwa.

Akamuuliza, "How do you feel Doctor?"

"Still very weak." Alijibu Mzee Makete.

"Expected. Most expected. You'll be as good as a new born in no time. You'll see." Chox akakichukua kipimamoyo na kuanza kumpima mgonjwa. Akasema. "Good. Very good. Very normal. Utahitaji sindano hii tu kwa jioni ya leo." Akaingiza mkono mfukoni na kutoa sindano na kichupa cha dawa.

Mzee Makete akasema, "Mpe mke wangu ani dunge."

Chox akasita.

"Ooh, usiwe na wasi wasi Dokta." Alisema Mama Denny akiinuka. "Mimi ni Nesi kamili. Wajua, ni mimi ninayemdunga sindano nyumbani."

"Good. Very good. Very good."

Chox akampa Mama Denny sindano na kichupa kile cha dawa. Akasema, "Just 2cc."

Mama Denny akaijaza sindano dawa, akakiweka kichupa mezani. Akainua sindano na kupunguza dawa, akitafuta usawa wa 2cc.

"Good. Very good. Exellent." Chox aliafiki akiiangalia sindano.

*****

Bessy, akikijaza kikombe cha chai, akauliza, "Ilikuwaje usiwe na msichana hadi makamo hayo?"

Dennis akakipokea kikombe akasema, "Huko ninakoishi wasichana warembo ni bidhaa adimu sana. Mno ni manyani tu."

Bessy, akakijaza kikombe chake. Akatabasamu na kuketi akauliza, "Unatarajia kuishi huko porini hadi lini?"

"Sijui." Denny alijibu. "Jana nilipoirudisha jeep na kuomba likizo ya dharura, Kanali aliniambia nakaribia kupewa Ukapteni na kuhamishiwa kitengo kingine."

"Kitengo gani?"

"Hakusema waziwazi ni kitengo gani. Lakini nashuku kitakuwa kitengo cha Busara - yaani Intelligence - Makao Makuu."

"Itakuwa safi sana. Tutakuwa tukionana mara kwa mara."

"Lakini patakuwa na mafunzo kwanza bila shaka. Pengine ng'ambo."

Denny akanywa funda la chai. Akauliza, "Wewe je?"

"Mimi kitu gani?"

"Imekuwaje usiwe na mvulana?"

"Ooh, nimeshafanya urafiki na wavulana wawili watatu. Mara mbili nilikaribia kabisa kufunga ndoa lakini mara zote nikaghairi dakika za mwisho."

"Kwa nini?"

"Kila mtu humwona ana walakini - maneno mengi, ahadi tele, mbwembwe, mikogo ... aa, unafiki mtupu!"

"Wasichana wengi huvutiwa na hayo." Alisema Denny

"Nao pia ni wanafiki." Alijibu Bessy.

"Au ni mazumbukuku."

"Mimi je? Ni mnafiki pia?"

"Ooh, wewe uko tofauti. Kwani mwenyewe hujioni ulivyo?"

"Kuna mtu anayejiona alivyo kikweli kweli?"

"Wapo." Alijibu Bessy. Kisha akaminya uso. "Lakini hapana. Nadhani ni kweli. Hakuna mtu anayeweza kujiona alivyo. Hao wanaodhani wanajijua walivyo wanajihadaa. Kila mtu hujiona mwema, mzuri. Hata Hitler, Amin na Mobutu walijiona wapo kama malaika."

Denny akakubali kwa kichwa akasema, "Hebu niambie. Umesema niko tofauti nikoje?"

"Ooh, uko kama nyani."

Wote kwa mara ya kwanza tangu wakutane wakacheka, kicheko cha dhati. Bessy akasema, "Hebu na wewe niambie, ni kitu gani kilichokuvutia kwangu?"

"Sijui." Alijibu Denny. "Labda kwa vile wewe ndiye mrembo wa kwanza na wa pekee kukutana naye tangu niachane na manyani wenzangu. Lakini nadhani hasa ni kwa sababu ya jeuri yako. Msichana mrembo kama wewe hupaswi kuwa jeuri hivyo."

"Mimi jeuri?"

"Mwenyewe hujijui?" Wakacheka tena. Baada ya kimya kifupi Bessy akasema. "Kwa hiyo tumekubaliana?"

"Ndiyo." Denny alijibu haraka.

"Chagua siku uipendayo. Mimi niko tayari kabisa. Nna hakika."

Bessy akaminya uso akauliza, "Unazungumzia nini wewe?"

"Harusi yetu."

"Idiot! Sijakwambia nakupenda. Sijakwambia niko tayari kuolewa na wewe."

Denny naye akakunja uso. "Kumbe unazungumzia nini? Tumekubaliana kitu gani?"

"Kwenda kupambana na Chiko."

"Aah! Hilo mbona tumeshalimaliza."

"Denny, huwezi kwenda peke yako."

"Sikiliza. Ngoja nikwambie mambo mawili. La kwanza, ninapotoa ahadi, iwe kwa Musa au Firauni sirudi nyuma. Na pili Chiko akiona tupo wengi atakimbia. Tutakuwa hatukufanya lolote."

"Sikiliza. Acha nichukue watu wawili au watatu tu. Watajibanza garini. Nitachagua watu wa uhakika."

Denny akatikisa kichwa. "No way, baby."

Bessy akakibamiza kikombe mezani na kufoka,

"Laanakum wewe! Laanakum wewe! Mbishi, mbishi kama -laanakum."

*****

Chiko aliipunguza mwendo pikipiki, akaiacha barabara kuu na kupinda kulia. Akaongeza mwendo na kutimua vumbi, akiukumbatia mkoba wa ngozi uliokuwa mbele yake kwenye tanki la petroli. Kiwanda cha zamani cha sukari kilikuwa kilometa nane kutoka barabara kuu. Kikiwa kimekufa miaka kadhaa nyuma. Kilichobakia ni magofu tu yaliyotelekezwa na kushambuliwa na wezi wa mabati, mbao, milango,vioo, madirisha na chochote kile chenye manufaa. Sasa yalikuwa magofu uchi, yapigayo miayo, yaliyonyukwa na mvua kadhaa za masika na jua kali la viangazi na kuzungukwa mbudu na ukoka. Upande wa kulia palikuwa na masalia ya majengo ya ofisi, na kushoto masalia ya korona na ghala, na katikati palikuwa na uwanja. Ilimchukua Chiko dakika chache tu kufika hapo, wakati jua likianza kuwa jekundu upande wa Magharibi. Akaiona pikipiki ya Fensy iliyoegeshwa mbele ya jengo la korona. Akaisimamisha pikipiki yake kando ya pikipiki ya Fensy. Akaizima na kuteremka, akiuchukua mkoba wake wa ngozi. Fensy akachomoza kwenye kona ya lango la korona. Chiko akamwuliza, "Mambo?"

"Poa kama jahannam," Alijibu Fensy.

"Hakuna chochote kilichotokea?"

"Si mtu, si jini. Upepo tu ukipiga miluzi kwenye haya magofu ya kichawi. Unaonaje, inawezekana asije?"

Chiko akaitazama saa yake. Akasema, "Tutaona baada ya robo saa. Kama ana chembe ya busara hatakuja." Akaufungua mkoba na kutoa SMG iliyokatwa kitako. "Au atakuja na kikosi. Nyuma kuko wazi?"

"Wazi kama jahannam - hakuna kikwazo,' Alijibu Fensy. Akaongeza, "Lakini nisingependa kuiacha pikipiki yangu, ingawa imechakaa."

"Hata mimi. Naamini hatutaziacha."

*****

Dennis aliitazama saa yake, akasema, ."Wakati na kuinuka."

Bessy akainuka pia, macho yamemuiva. Akasema, "Denny, uwe mwangalifu tafadhali."

"Ndiyo, nitakuwa mwangalifu." Alisema Dennis. "Sikiliza, usitoke hapa. Kuwa karibu na simu. Ukiona kimya hadi saa kumi na moja na nusu chukua kikosi mje kiwanda cha zamani cha sukari . Niahidi utafanya hivyo, na si lolote jingine."

# 11

## *Kilingo cha mwisho*

Dennis akawasili kwa kasi kiwanda cha zamani cha sukari, akitimua vumbi. Akaziona pikipiki zilizoegeshwa mkono wa kushoto, akaliserereshა
gari mkono wa kulia. Likaenda kutulia mbele ya gofu lamwisho, mabaki ya ofisi ya meneja wa ki- wanda hapo zamani. Akaufungua mlango wa gari, akachupa na ku- jibiringisha, akifuatiwa na mvua ya risasi za SMG. iliyokuwa ikichakarika kwenye lango la korona. Alipopenya tu ndani ya gofu hilo, Denny akainuka, akaichomoa bastola na kuangaza haraka humo ndani. Uwazi wa mahali lilipokuwa dirisha la nyuma ukamkenulia. Akauruka na kusimama nyuma ya gofu, akisikiliza kwa makini.

Kwa nukta kadhaa kote kulikuwa kimya isipokuwa kuvuma kwa upepo. Kisha akaisikia sauti ya Chiko ikiita kwa mbali. "Hey! School Boy! Niko hapa."

Denny akatambaa kinyoka kwenye majani yaliyolizunguka gofu hilo akachomoza kichwa na kuliona gofu la korona. Akamuona Chiko akizungumza na kumfanyia ishara mwenzake. Kisha akaachia risasi za mfululizo, akilishambulia gofu la ofisi. Wakati huo huo Fensy akatoka mbio, bastola mkononi, akilifuata gari. Akachungulia ndani, akitazama kama mlikuwa na watu waliojificha. Kisha akanyata, akajibanza na kuchungulia ndani ya gofu kiwandani. Alipohakikisha · liko tupu akapenya ndani kwa tahadhari. Ali pofika katikati ya uwanja, Denny akainuka hari, bastola ikilenga mbele. Denny akajikunja na kumfuata. Akamkuta akihungulia kwenye uwazi wa dirisha. Ingekuwa rahisi sana kumrukia, hata kama Denny asingekuwa na silaha Lakini badala yake, akamwamuru "Ganda."

Fensy hakuganda. Alishtuka, akageuka kwa kasi, akiachia risasi ovyo. Zote zilipita juu, kwani Denny alikuwa amechutama. Akaachia risasi mbili zikamsomba Fensy mzima mzima na kumrusha nje ya uwazi wa dirisha na kudondoka chini kwa kishindo. Denny akageuka na kuchungulia njee kwenye gofu la Korona. Kote kulikuwa mkima kumetulia tulii, isipokuwa upepo ukipeperusha vumbi. Akatambaa hadi nyuma ya gari na kujibanza, Akaukinza mdomo kwa vyiganja vyake ana kuita, "Chikooo."

Chiko akachomoza uso kwenye lango la Korona na kuita, "fensy vipi?"
Denny akalitambua kosa la Chiko alimdhania kuwa ni mwenzake. Denny akaamua kubahatisha, akaukiza tena mdomo wake na kusema "Tayari mshenzi kaniumiza mguu."
Chiko akasita kidogo kisha akachomoza SMG mathubuti mikononi akaanza kutembea kwa tahadhari macho yake na mdomo wa mtutu kwenye mlango wa mabaki wa ofisi ya meneja. Alipofika katikaiti ya uwanja Denny akaenuka ghafla nyuma ya gari, mdomo wa bastola ukikilenga kichwa cha mkora huyo. Akamwamuru, "Dondosha"
Chiko akaganda, akageuza kichwa, akatoa macho kwa mshangao wa dhati. Akanong' ona kama anayeota, "School Boy!"
"Ndiyo." Denny alimjibu. "Ni School Boy yuko darasani. Dondosha hiyo bunduki."

* * * * *

Bessy aliposema angevuja jasho kila nukta ya nje ya dakika hizo zote hakuwa akidhihaki. Kwa sababu - kama hapakuwa na sababu yoyote nyingine ya maana - kwa sababu kama Dennis angefikwa balaa lolote huko kiwanda cha zamani cha sukari, yeye Bessy angewajibika. Akiwa afisa wa polisi hakupaswa kumwacha mtu ahatarishe maisha yake kwa kupambana na magaidi wa hatari. Hata kama mtu huyo alikuwa ni komandoo wa Jeshi la Ulinzi. Hii ilikuwa ni kazi ya polisi. Hivyo sasa Bessy alikuwa anajuta.
Muda wote huo akitokwa jasho. Na hakuweza kutulia. Mara aketi, mara ainuke na kutembea tembea hapo sebuleni. Na wakati wote mara aiangalie saa yake, mara aiangalie simu, huku akihimiza, "Come on boy! Come on boy! Come on boy!" Hivyo, simu ilipolia, jinsi alivyoruka ni kama aliyegusa umeme. Haishangazi. Akaunyakua mkono wa simu na kusema, "Hallo! Denny!"
"Bessy?"
Haikuwa sauti ya Denny bali ya Kamishna Msaidizi wa polisi. "Bessy. Mbona hujaripoti mpaka saa hizi?"
Bessy akakumbwa na fazaa. Akababaika, "Mzee, Mzee, nna - nnamsubiri Denny"
"Kwa nini?"
"Amekwenda - amekwenda ki wanda cha zamani cha sukari."

"Kufanya nini?"
"Kukutana na Chiko."
"Mbona sikuelewi, Bessy!" Alisema Kamishna' Msaidizi. "Unazungumzia kitu gani?"
"Ooh, samahani sana kwa kukuficha Mzee. Ukweli ni kwamba Denny ana kichwa kigumu sana. Amepatana na Chiko kukabiliana huko kiwanda cha sukari, na amekataa kufuatana na mtu yoyote."
"Mungu wangu, Bessy! Umeruhusu kitu kama hicho?"
"Ningefanya nini, Mzee? Amesema hakuna njia nyingine. Vinginevyo tutamkosa Chiko, na yeye ni Komandoo."
"Hata angekuwa nani!" Kamishna Msaidizi alifoka. "Yeye si polisi. Ni afadhali kumkosa huyo mlaaniwa kuliko kuhatarisha maisha yake. Akiumia sisi wote tutaonekana wazembe wakubwa! Sikiliza. Jitayarishe. Natuma watu watatu wakupitie."
"Lakini Mzee, nimemwahidi sitafanya lolote hadi saa kumi na moja na nusu."
"Sitaki kusikia upuuzi wowote. Gari litakuwa hapo baada ya dakika mbili au tatu tu."
Simu ikakatwa. Bessy akapumua. Kwa upande alifurahi. Kwani alikuwa akitii amri ya mkuu wake, hakuwa akivunja ahadi kusudi.
Alipomaliza kufunga milango tu akasikia king'ora cha gari la polisi likija kwa kasi.

*****

Chiko akasita, macho yake yakizungumza waziwazi mawazo yake. Alikuwa akikadiria ingemchukua sehemu gani ya sekunde kuugeuza mdomo wa bunduki mzunguko wa nyuzi kama ishirini au thelathini, na ingemchukua Denny sehemu gani ya nukta kukivuta kilimi cha bastola yake iliyokuwa imemlenga.
Kisha akayaona macho ya Denny yanavyowaka.
Akasisimuka mwili mzima na kuibwaga SMG.
Ulikuwa mtego. Denny naye akaidondosha bastola na kuanza kumfuata kwa hatua za pole pole, macho yao yameumana.
Alipobakiza hatua kama tano, Chiko kwa kasi ya chui akaichupia SMG. Vidole vyake vilikwishagusa chuma alipofumuliwa teke la kifuani lililompindua chali.

"Inuka." Denny alimwamuru.

Chiko akakurupuka kama nyati aliyejeruhiwa.

Akakutana na teke la mzunguko lililombwaga kifudifudi. Denny akamkwida ukosi na kumwinua. Akamzungusha na kumnyuka ngumi nne za mfululizo. Chiko akapepesuka. Akakung'uta kichwa kuondosha ulevi na nyota zilizomzonga. Akajizatiti na kukumbuka yeye ni nani. Akakurupuka tena! Akarusha ngumi, akarusha teke. Vyote viliambulia patupu.

Akajirekebisha na kujaribu kujiweka sawa. Akarusha ngumi, akarusha teke kwa mara nyingine. Akajikuta anakata tena hewa na kuzidi kujichosha. Denny akajizungusha na kumfumua teke la juu kwa juu. Chiko akapepesuka.

Akafumuliwa tena teke la usoni. Akadondoka 'puu' kama gunia la mchanga. Alipotaka kuinuka Denny akamkanyaga kwa nguvu kwenye uti wa mgongo. Mfupa ukalia 'ko', Chiko akapiga yowe na kurudi chini kifudifudi.

"Huo," Denny akamwambia, "ni mfupa wa kiuno. Ili kuhakikisha huinuki tena katika maisha yako yote. Wala huketi. Wala huchutami. Wala hutambai. Sasa wewe ni mtu wa kubebwa na kugeuzwa tu kama maiti. Na huo ni mwanzo tu." Denny alimfahamisha. Akamuuliza kwa ukali. "Wapi anaishi Kassim Hashir?"

"Go to hell."

"Hajahamia huko bado." Denny akamnyuka teke la mdomoni. Chiko akatema damu na meno mawili.

"Wapi nitampata Kassim Hashir?"

"Nakwambia simjui jamaa huyo." Chiko alililoloma.

"Namtaka mtu aliyemgonga babangu. Na utanambia tu alipo, pamoja na ubabe wako. Ikibidi nitakungoa meno yote. Na kisha niivunjevunje mifupa yako yote."

"Nakwambia aliyemgonga babako haitwi hivyo."

"Potelea mbali anaitwaje?. Nataka kujua anakoishi." .

"Sikujui anakoishi."

"Sikuamini."

"Shauri yako."

Chiko akala teke jingine na kutema jino jingine.

Akaloloma, "Nakwambia kweli. Sijui anakoishi. Nilikwenda kwake mara moja tu, tena usiku. Huko Buffalo Hill."

"Ulifikaje?"
"Nilipelekwa na ... na ... "
"Na nani?"
Chiko akabaki kimya. Denny akainua mguu, lakini Chiko akamzuia. "Subiri! Nilipelekwa na Kembo. Sam Kembo."
"Ndiye nani huyo?"
"Rafiki yake huyo aliyemgonga babako."
"Yaani ndiye mtu wa kati baina yenu na huyo Kassim Hashir?"
"Ndiyo."
"Nitampata wapi?"
"Sijui."
Denny akaanza kulitayarisha teke.
"Subiri!" Chiko akasema haraka. "Anatusubiri Flamingo Guest House, chumba Namba 202."
"Kama unanidanganya, ole wako. Nitakurudia. Na ujue nitakukuta hapa hapa, hivyo hivyo ulivyo."
"Kwa nini nikidanganye? Mimi nimekwisha, kwa nini wao wapone?"
Denny akaifuata bastola. Alipoinama aiokote akasikia kingora cha gari la polisi. Akaiokota, akageuka na kuitazama barabara.
Golf ilikuwa ikija kasi, ikitimua vumbi. Ikaserereka na kusimama. Bessy akatoka mbio, akaita "Denny!" Akajitupa kwenye kifua cha Denny, huku akicheka na akilia wakati huo huo.
Denny akampigapiga mgongoni, akimwambia,
"It's okay baby. It's okay." Akawatazama askari watatu wakitoka garini, kila mmoja kakumbatia SMG. Akawaambia, "Naona mmechelewa kidogo mabwana. Mchezo umekwisha. Majeruhi huyo hapo, na mzoga uko nyuma ya gofu lile."
"Ni wao wawili tu?" Askari mmoja aliuliza.
"Ni wao tu."
Askari mmoja akamwendea Chiko na kumtek-enya kwa kiatu. "Hey, wewe! Inuka twende."
"Siwezi." Chiko alilalama. "Mwanakharam kanivunja kiuno."
Bessy akamtazama Denny, macho yake yakimshutumu.
"Kaniita School Boy."

"Hilo ni tusi kubwa?"
"Akh, shika!" Akamkabidhi bastola yake.
"Twende zetu. Kuna kazi ya kufanya."
"Wapi?" Bessy aliuliza, wakielekea kwenye gari.
"Flamingo Guest House. Kukanyaga ngazi ya mwisho. Mtu mmoja aitwaye Sam Kembo." Denny akaliwasha gari na kuling'oa. Akasema, "Kwa hiyo hukuweza kusubiri hadi saa kumi na moja na nusu?"
"Hapana, nimelazimishwa na Kamishna Msaid-izi nikufuate pamoja na wale askari watatu. Lakini nilifurahi. Jinsi nilivyokuwa nikitokwa jasho ningerukwa akili."
"Ndiyo maana unanukia vizuri zaidi. Nitakufanya utokwe jasho kila siku."
"Shetani mkubwa we."
Baada ya kimya kifupi Bessy akasema, "Nasikitika kufanya kile kitendo cha kipumbavu mbele ya wenzangu. "
"Kitendo gani?" Denny aliuliza.
"Kule kukuvamia nilipoona uko salama."
"Hakikuwa kitendo cha kipumbavu. Ulionyesha jinsi unavyonipenda. Ulinifurahisha sana."
"Sikukuvamia kwa sababu ya kukupenda, you idiot. Nilifurahi kukuona uko salama. Ungeumia ningefukuzwa kazi."

*****

Punde akalisimamisha gari nje ya Flamingo, picha ya ndege huyo, korongo mweupe aliyesimama kwa mguu mmoja, ikipatangaza mahali hapo.
Wakazipanda ngazi hadi ghorofa ya pili. Mbele ya mlango wenye nambari 202 Denny akamfanyia ishara Bessy abishe. Akaugonga mlango.
Sauti nzito ikauliza, "Nani?"
"Ni mimi." Bessy alisema kwa sauti laini ajabu. "Nifungulie."
Mlango ukafunguliwa kidogo. Denny akaupiga kikumbo na kuingia nao ndani. Huku akipepesuka kwa hicho kikumbo, Kembo akaupeleka mkono wake ndani ya koti.
Denny akamkwida na kumbamiza ukutani. Akamnyang'anya bastola aliyokuwa akiitoa. Akamzungusha na kumsukumia mlangoni. "Twende."
"Wapi?" Kembo aliuliza, akijifuta damu mdomoni. "Nyie ni nani?"

"Ni Inspekta Bessy na Dennis Makete. Tupeleke kwa rafiki yako, Kassim Hashir."

"Simjui mtu huyo."

Denny akamnyuka kofi la kelbu. "Usimwige Petro."

"Ndiye nani Petro?"

"Jesus Christ! Hata Petro humjui! Ni Mkristo kweli wewe?"

"Sikiliza," Kembo alihema kwa nguvu. "Sikilizeni. Mimi si mtu wa ghasia."

"Alaa! Ndiyo maana ukawatuma akina Chiko wakufanyie ghasia zako?"

"Chiko!" Kembo aliguna kizembezembe. "Yuko wapi Chiko?"

"Nilidhani utasema naye pia humfahamu!" Denny alisema, akiufungua mlango na kumsukuma Kembo nje. "Chiko na Fensy wako wanakostahili kuweko, jehannam."

Wakaziteremka ngazi. Chini Denny akamrushia Bessy funguo za gari. "Endesha wewe." Alimwambia. "Sisi tutastarehe kwenye siti ya nyuma na huyu rafiki yangu."

Wakaingia garini. Bessy akalitia moto. Akauliza, "Buffalo Hill?"

"Buffalo Hill." Denny alimjibu. Akamtekenya Kembo kwa mdomo wa bastola yake mwenyewe.

"Mtaa gani?"

"Kitosi." Kembo alijibu bila ya kusita.

"Namba?"

"Ishirini na moja."

*****

"Wageni wa Mzee, fungua geti." Akiwa kawekewa na Denny bastola yake mwenyewe ubavuni, Kembo alimwamuru mlinzi baada ya kumwona kusita kidogo kutokana na sura alizoongozana nazo kuwa ngeni machoni mwake.

Haoo, wakajitoma ndani. Bessy akalisimamisha Bentley nyuma ya Benz jeupe, mbele ya jumba hilo la kifahari. Wote watatu wakateremka. Waki-ongozwa na Sam Kembo aliyekuwa akisukumwa, wakaingia ndani.

Kassim Hashir, kwa jina jingine Habib Kessy' alikuwa ameketi sebuleni raha mstarehe. Akinywa na kuvuta, huku kakipakata kisichana cha miaka kumi na mitatu au kumi na mine wakitazama video ya picha chafu kwenye skrini ya upana wa dirisha kubwa. Akainuka ghafla, akijimwagia kinywaji chake, akisema kwa mshangao mkubwa, "Sam Vipi? Imekuwaje?"

"Hawa vijana wana shida nawe." Kembo alisema kwa sauti kavu na chovu. "Kachero Inspekta Bessy na Dennis Makete."

"Karibuni." Alisema Kassim haraka, akiilazimisha sauti yake iwe thabiti na ya kirafiki. Na alikaribia kufaulu.

Hakuna aliyeketi.

Denny akasema. "Wewe ndiye Kassim Hashir?"

"Hapana. Umekosea. Mimi ni Habib Kessy."

Bessy akauliza, "Wa H.K. International?"

Kassim akasita kidogo tu kisha akakubali haraka.

"Ndiyo. Wa H.K.International. Umejuaje?"

"Wizara ya Biashara na Viwanda imetuomba tuichunguze kampuni yako. Lakini kazi hiyo sikupewa mimi .... Ningegundua tu kama wewe ndiye Kassim Hashir."

"Lakini mimi siye Kassim Hashir."

"Wewe ndiye uliyemgonga babangu jana asubuhi" Alisema Denny.

"Hapana, ni mtumishi wangu aliyemgonga. Acha nimwite. Atakiri mbele yenu. Anasema ilikuwa bahati mbaya. Alifanya upumbavu mkubwa kutokwenda polisi kuripoti. Msingesumbuka hivi."

"Babangu alikuona."

"Kumradhi ?"

"Babangu alikuona kabla ya kumgonga. Akakutambua, anasema ulimgonga kusudi."

"Akh! Kwa nini nifanye kitu kama hicho? Kwa maslahi gani? Mimi simjui baba yako. Sijawahi kukutana naye hata siku moja."

"Labda hukuwahi kukutana naye kabla ya hapo jana lakini una uhusiano naye. Tena mkubwa sana."

"Mimi na Dokta Makete tuna uhusiano?"

"Ndiyo. Ulianza zaidi ya miaka ishirini na tano iliyopita, kutokana na msichana aitwaye Asha Rajabu."

"Asha Rajabu? Ndiye nani huyo?"

"Alikuwa msichana wa skuli. Ukampa mimba."

"Ooh, nasikitika sana, ilikuwa bahati mbaya, bila ya shaka. Lakini tena, hilo si jambo la ajabu kwa wakati huo na hata hivi sasa. Wasichana wa shule hupata mimba kila siku."

"Ni kweli, si jambo la ajabu." Alikubali Denny, "isipokuwa ulimwambia akaitoe."
"Oh, bila shaka sikupenda aharibu masomo yake." Alisema Kassim Hashir.
"Ulimpa kikaratasi cha kumuamuru daktari wa zamu aitoe mimba hiyo. Daktari wa zamu alikuwa babangu, Dk. Raymond Makete. Akakataa. Akamshauri Asha arudi nyumbani na kuitunza mimba."
"Ulikuwa ushauri wa busara."
"Ndiyo, ulikuwa ushauri wa busara." Denny alikubali. "Ni kweli msichana huyo hakurudi kwako. Alienda kwao. Lakini mimba ilipokuwa kubwa
babake akagundua. Akamfukuza Asha nyumbani. Msichana huyo akawa hana pa kwenda isipokuwa kwa mjomba wake. Tatizo hakuwa na nauli. Akaja kukuomba wewe pesa."
"Nilimsaidia, bila ya shaka?"
"Sana! Ulimsaidia sana. Kwa kumchoma kisu tumboni mara mbili."
"Ooh, God!"
"Kisu kimoja kilinipata hapa." Denny alisema, akilirarua shati lake na kulifichua kovu la begani.
"Na kisu kingine kikanipata takoni."

*****

Nukta moja sebuleni pakawa kimya kabisa. Nukta ya pili Kassim Hashir akaruka kimanga kama aliyekanyaga moto. Kufumba na kufumbua akawa na bastola mkononi, na akilenga. Kifua wazi, Denny akamshika Kembo na kum sukuma. Akapachikwa risasi mbili. Moja kifuani upande wa kushoto, ya pili kwenye paji la uso. Zikamsomba hadi kwenye zulia, akajipindua mara mbili tatu kabla hajatulia tuli. Denny na Bessy walikwishachupa nyuma ya sofa, bastola mkononi. Lakini Kassim alikuwa akikimbilia nje, huku akiendelea kurusha risasi ovyo. Akaingia ndani ya Benz akaliwasha na kuling' oa kwa pupa, magurudumu yakichacharika na kutoa moshi.
Denny akatoka mbio, akimpuuza Bessy aliyekuwa akitaka asubiriwe. Akaingia ndani ya Bentley na kuliandama Benz lililokuwa likipenya getini na kupinda kushoto. Magari yote mawili, moja likiwa limeundwa na Mjerumani na jingine na Mmarekani, yalikuwa mazito yenye nguvu karibu sawa. Na wote wawili, Dennis Makete na Kassim Hashir walikuwa madereva mahiri. Hivyo

kwa zaidi ya robo saa magari yote mawili yalikuwa kama yaliyo kwenye mbio za mashindano ya kuonyesha nani zaidi kati ya madereva hao kama siyo kati ya Mjerumani na Mmarekani. Muda wote yakiwa yameachana kwa karibu umbali ule ule wa kama mita ishirini na tano hivi.

Kisha wakaanza kuukwea mlima Katahewa, wenye kona mbaya, miinuko na miteremko ya ghafta, na madaraja marefu lakini membamba. Pande zote za barabara zilijaa alama za kutahadharisha madereva, waendeshe pole pole na kwa uangalifu. Lakini kati yao, hakuna aliyepunguza mwendo.

Magari waliyopishana nayo ilibidi yajibanze pembeni, madereva wa magari hayo wakishangaa na kulaani.

Kidogo kidogo Bentley likalinyemelea Benz. Kassim Hashir akaanza kuliyumbisha gari lake, kuziba njia ili asipitwe. Hata hivyo, baada ya juhudi kadhaa, Denny alifanikiwa kuipenyeza pua ya Bentley na kuligusagusa Benz ubavuni usawa wa tanki 1a petroli.

Katika hali hiyo, ghafta, mita kadhaa mbele yao pakajitokeza daraja refu na jembamba, na mporomoko wa zaidi ya mita mia bondeni. Ilikuwa wazi magari hayo mawili yasingeweza kulivuka daraja hilo sambamba. Lakini hakuna aliyepunguza mwendo. Denny akavuta pumzi ndefu, akakanyaga mafuta hadi mwisho, akililenga daraja, kidogo kidogo akilisukuma Benz nje ya barabara. Kassim Hashir akaitumia fursa hiyo kuchomoa bastola yake na kumlenga Denny. Akaishia kujisemea mwenyewe, "Shit! Damn shit!" Risasi zote alikuwa kazimaliza wakati akichacharika kukimbilia kwenye gari na wakati akiling'oa gari lake. Denny alikwishaligundua hilo mapema hivyo hakujisumbua hata kujaribu kukwepa. Kufumba na kufumbua gari moja likalivuka daraja na jingine likaelea hewani.

Denny akafunga breki ng'ambo ya daraja, akateremka na kusimama akiliangalia Benz lina vyobiringika kwenye mporomoko, kama kigari cha bandia. Ghafla likalipuka na kushika moto, hatimaye likagota bondeni na kutulia, likiendelea kuwaka.

Denny akataka kurudi garini aondoke, mara akasikia mayowe huko bondeni. Akaona mtu anayewaka akitoka katikati ya moto, akipiga mayowe na akihangaika ovyo. Haikuhitaji kuambiwa kuwa nguo za Kassim Hashir zilikuwa zimeloa petroli chapachapa. Zikapita nukta kadhaa, Denny akasikia milio kwa mbali kama filimbi. Mara ikaanza kukaribia na kusikika vyema

zaidi. Vilikuwa ni ving'ora vya magari ya polisi. Yalikuwa mawili. Kwenye gari la kwanza akateremka Bessy na Kamishna Msaidizi wa polisi. Wakamfuata Denny. Wakasimama kimya kando yake wakimwangalia mtu aliyekuwa akiwaka, akipiga mayowe na kutapatapa.

Kisha Bessy akauliza kikondoo kondoo, "Kassim Hashir?"

Denny akakubali kwa kichwa, na kuongezea, "Ndiye. Kassim Hashir."

"Safari hii," msichana akasema, "Atazikwa yeye mwenyewe. Au masalia yake, na siyo kivuli chake."

Kamishna Msaidizi ambaye muda wote mawazo yake yalikuwa yametekwa na gari lililokuwa likiteketea bondeni akawasogelea akisema huku akitikisa kichwa kwa masikitiko. "Hasara iliyoje!" Ilikuwa ni kama nusu akiwaambia Bessy na Denny lakini mno alijiambia mwenyewe. "Lilikuwa gari zuri sana. Tunawakataza kuendesha wakiwa wamelewa lakini wapi, hawasikii!"

Bessy akamshika mkono Denny.

"Twende zetu It's all over now. MSAKO WA HAYAWANI umekwisha."

Wakaingia kwenye Bentley.

Denny akaligeuza na kulielekeza jijini.

Bessy akauliza, "Utanipiga konzi la wapi?"

"Utachagua mwenyewe," Denny alijibu kwa sauti chovu na kuongeza mwendo. Alikuwa akilikumbuka swali alilomuuliza Chiko kule kiwanda cha sukari.

"Wapi anaishi Kassim Hashir?"

Najibu la huyo mkora.

"GO TO HELL."

# MWISHO